# BWANA NDIYE MCHUNGAJI WANGU

Zab. 23, (K) 1

Shanel Komba
28.03.2011
Dodoma

**Wimbo wa Katikati**
**Jumapili ya 4, Kwaresma A**




2. Hunihuisha nafsi yangu na kuniongoza/ Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.

3. Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti sitaogopa mabaya/
   Kwa maana wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyanifariji.

4. Waandaa meza mbele yangu, machoni pa watesi wangu/
   Umenipaka mafuta kichani pangu, na kikombe changu kinafurika.

5. Hakika wema na fadhili zitanifuata, siku zote za maisha yangu/
   Nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele.

6. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu/
   Kama mwanzo na sasa na siku zote na milele Amina.